

**ATHARI ZA MFUMO WA VIHUSISHI VYA KINANDI KATIKA  
UAMILIAJI WA KISWAHILI KAMA L2 MIONGONI MWA  
WANAFUNZI WANAOSEMA KINANDI KAMA L1**

*Susan Chebet-Choge*

**Ikisiri**

*Uamiliaji wa L2 ni tukio lisiloepukika katika karne ya sasa yenye migusano mingi ya lugha inayosababishwa na mitagusano ya watu wanaosema lugha tofauti na kupitia ujifunzaji na ubwiaji wa lugha. Uamiliaji wa L2 ni zao la maendeleo ya binadamu, kijamii, kiuchumi na kisiasa. Maendeleo haya hulazimisha nchi na watu kujifunza lugha nyingine ili mahitaji fulani ya maendeleo yaweze kuafikiwa. Uamilijia huu unakuwa wa lazima ili watu wanaosema lugha tofauti waweze kuelewana na kubadilishana mawazo. Mwamiliaji wa L2 mara nyingi hukumbwa na changamoto ya kuathiriwa na mfumo wa kiisimu wa L1. Athari kutoka L1 ni za kifonetiki, kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki, ambazo zinamwaathiri mwamiliaji wa L2. Makala hii imeshughulikia athari za kimofosintaksia za mfumo wa vihusishi vya Kinandi katika insha za Kiswahili za wanafunzi wanaosema Kinandi kama L1. Ni zao la utafiti uliofanywa katika shule tatu za msingi katika Kaunti ya Nandi nchini Kenya kwa minajili ya kuandaa tasnifu ya uzamili. Katika utafiti huo, shule hizi zilirejelewa kwa akronimu NSB. Utafiti huo ulibainisha changamoto nyingi za kiisimu-nafsia katika kiwango cha kimofosintaksia zinazomkumba mwanafunzi anayesema Kinandi kama L1 anapoamilia Kiswahili kama L2. Mojawapo ya vyanzo vya changamoto hizi ni athari za mfumo wa vihusishi vya Kinandi zinazojadiliwa katika makala hii.*

**Utangulizi**

Uamiliaji wa L2 umefanyiwa utafiti na kufafanuliwa kwa mitazamo tofauti na wataalamu mbalimbali. Baadhi ya wataalamu hao wametafiti jinsi mtu anavyoamilia L2 kupitia ubwiaji wake sambamba na ule wa L1 ama baada ya L1 (Van Els n.w, 1997, p. 34). Krashen (2009, p. 114), kupitia nadharia tete ya modeli-

kisimamizi, anatofautisha kati ya ubwiaji na ujifunzaji wa lugha. Kwake, ubwiaji ni kule kupokea lugha pasipokufunzwa na ujifunzaji ni mchakato unaompokeza mtu ujuzi wa lugha kupitia yeye mwenyewe kujifunza ama kufundishwa kama inavyofanywa shuleni na vyuoni. Naye Yule (2010, p. 187) anasema kuwa, ubwiaji unarejelea upokezi wa lugha kihatua kupitia matumizi yake katika mawasiliano ya kawaida nao ujifunzaji kama mchakato unaotambuliwa na mjifunzaji na hutekelezwa kupitia mafundisho ya msamiati na sarufi ya lugha lengwa. Kutokana na maelezo haya, mtu hupokea lugha ya pili kupitia mpangilio mahususi kama inavyofanywa katika taasisi za masomo ama kupitia ubwiaji kutoka katika mazingira yake ya kimatumizi.

Utafiti uliofanywa miongoni mwa wanafunzi wanaosema Kinandi kama L1 katika shule za msingi za NSB na ambayo makala hii inaripoti baadhi ya matokeo yake, ulibainisha kuwa; mfumo wa kimfosintaksia wa Kinandi unawaathiri wanafunzi hao wanapojifunza Kiswahili kama L2, kama ilivyodhihirika katika mfumo wa vihusishi katika insha zao.

Vihusishi hutekeleza jukumu kubwa katika lugha la kufungamanisha vipengele tofauti vya kisintaksia ili tungo iweze kueleweka na kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa. Hivyo basi, ni vifaa vya ushikamano katika lugha. Vihusishi vikitumiwa vyema, muwala na ushikamano wa matini huafikiwa. Vihusishi hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine kwa aina na idadi japo vinatekeleza takriban kazi sawa. Mwangi (2003, p. 57-61) akiwarejelea wataalamu Rauh, Huddleston, König & Kortman, Vestergaard na Quirk n.w. miongoni mwa wengine, anasema kuwa, katika lugha zingine, vihusishi ni seti fungu inayotekeleza kazi ya kimuundo na havibadiliki, ilhali katika lugha zingine, vihusishi ni seti kati-iliyofunge na isiyofunge- na huathiriwa na mabadiliko kama vipengele vingine vya lugha. Vilevile, katika lugha zingine, vihusishi vina dhima ya kileksia, kudhihirisha kuwa, vinaweza kubadilisha maana katika baadhi ya miktadha inapotumiwa na katika mtindo wa M-4, vihusishi ni aina mojawapo ya mofu-mfumo vukio. Matumizi yake huchochewa na mofu za mada na mofu-mfumo mawio panapotokea

haja ya kuundwa kwa vipashio vikubwa zaidi vitakavyoweza nia ya mnenaji ieleweke kwa uwazi na kwa kina (Choge, 2016, p. 146).

### **Nadharia zilizoongoza utafiti wa makala hii**

Makala hii imeongozwa na nadharia mbili; ya kwanza ikiwa, nadharia ya **Muundo wa Lugha MFumo** ambayo kuanzia hapa katika makala hii, imejulikana kwa akronimu **MLF** na Mitindo yake Saidizi ambayo ni **Mofu 4** na **Kiwango Dhahania** ambayo imejulikana katika makala hii kwa akronimu **M-4** na **KD** mtawalia. Nayo nadharia ya pili ni Uchanganuzi Linganishi.

### **Nadharia ya MLF na Mitindo yake Saidizi**

Nadharia ya mtindo wa **MLF** na Mitindo yake miwili saidizi ya **M-4** na **KD** iliasisiwa na Myers-scotton na wenzake katika miaka ya 1990 (Choge, 2018, p. 113-114; Myers-Scotton, 2002, p. 54-96, Myers-Scotton, 2001a, p. 87-90). Waliibua mtindo wa **MLF** ili kuelezea jinsi lugha zilizomo katika mitagusano zinavyoshirikiana katika kuzalisha tungo kengeushi zilizochangiwa kiisimu na lugha zinazoshiriki. Tungo Kengeushi ni tungo ambayo imekiuka usanifu wa kimofosintaksia wa lugha inayotumiwa katika mawasiliano kutokana na athari za lugha nyingine. **M-4** ni mtindo saidizi wa kwanza kuibuliwa ili kuusaidia mtindo wa **MLF** katika kuelezea jinsi mofu za lugha zilizo katika mtagusano zinavyochangia tungo kengeushi iliyochangiwa kiisimu na lugha zinazoshiriki (Myers-Scotton, 2008, p. 22-24). Mtindo saidizi wa pili ni **KD** ambayo ulibuniwa ili ueleze jinsi tungo kengeushi inavyotiwa usanifu fikirani mwa mnenaji/mzalishaji tungo kulingana na mfumo wa **LM**.

Mtindo wa **MLF** unaeleza kuwa, lugha zote zinazoshiriki katika kuzalisha tukio la kiisimu lililochangiwa na lugha mbili ama zaidi kiisimu hutekeleza majukumu tofauti. Mojawapo ya lugha hizi huchukua jukumu la Lugha Mfumo (**LM**) na nyingine Lugha Leksishi (**LL**). **LM** inaongoza upatanisho wa kisarufi ilhali **LL** huchangia leksia katika tungo husika. Katika miktadha mingine, lugha zinazoshiriki hubadilishana majukumu haya. Mtindo wa **M-4** una aina nne za mofu katika tungo ya kisintaksia (Choge, 2018, p. 115; Choge, 2016, p. 17-23). Mofu hizo zimo katika makundi mawili ambayo ni *mofu za mada* (**MD**) na *mofu za mfumo* (**MF**). Mofu za mfumo zimegawanywa tena katika vikundi viwili ambavyo ni *mofu-mfumo mawio* (**MFM**) na *mofu mfumo limatia* (**MFL**). Nacho kikundi cha mofu limatia kimegawanywa zaidi kwa vijikundi viwili ambavyo ni; *mofu mfumo limatia vukio* (**MFLV**) na *mofu mfumo limatia tazama nje* (**MFLN**). *Mofu za mada* huteuliwa fikirani na hubeba nia ya mnenaji/mzalishaji tungo. Nazo *mofu za mfumo* huweka

usanifu wa tungo kulingana na sarufi ya LM. *Mofu-mfumo mawio* huteuliwa fikirani ikiwa mofu za mada zinahitaji maelezo zaidi ili fikra za mnenaji/mzalishaji wa tungo zieleweke. Nazo *mofu-mfumo limatia* hutukia iwapo vipashio vikubwa vinahitajika kuundwa nazo mofu-mfumo limatia vukio hutukia iwapo mofu za mada zinahitaji kipashio kikubwa ili nia ya mnenaji/mzalishaji wa tungo iweze kuafikiwa. Maana na ufafanuzi juu yazo hupatikana ndani ya kipashio kinachozibeba. Nazo *mofu-mfumo limatia tazama nje* hutukia kwa minajili ya kuleta ushikamano wa tungo. Hutazama nje ya kipashio kinachozibeba kwa maelezo zaidi kuihusu (Choge, 2018, p. 116). Nadharia hii ilituwezesha kutambua na kuelezea majukumu ya Kinandi na Kiswahili katika tungo kengeushi kwenye insha za wanafunzi zilizochanganuliwa. Jedwali lifuatalo linaonesha mpangilio wa mofu hizi nne.

Jedwali 1: mpangilio na uhusiano wa mofu za mtindo wa M-4

MPANGILIO WA MOFU ZA M-4				
Makundi ya M-4	Maelezo ya mofu za M-4	Na. za mofu za M-4		
1	Mofu za Mada (MD)	1		
2	Mofu za mfumo (MF) ( <i>ni za aina mbili</i> )	#		
	<b>Aina za MF</b>			
	2 (i)	Mofu za mfumo mawio (MFM)	2	
	2 (ii)	Mofu za mfumo limatia (MFL) ( <i>ni za aina mbili</i> )	#	
		<b>Aina za MFL</b>		
		2 (ii) a	Mofu za mfumo limati vukio (MFLV)	3
		2 (ii) b	Mofu za mfumo limati nje (MFLN)	4

Imetoholewa kutoka (Choge, 2018, p. 116)

### ***Nadharia ya uchanganuzi linganishi***

Kando na kutumia nadharia ya MLF na mitindo yake saidizi , makala hii ilitumia pia Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi iliyoasisiswa na Fries na Lado mnamo 1945 na 1957 mtawalia na baadaye ikaendelezwa na wataalamu tofauti kama *nadharia tete* ama *nadharia* (Dost & Bohloulzadeh 2017; Al-khresheh, 2016). Nadharia (tete) hii imetumika kwa muda mrefu kutafitia nafasi ya L1 katika ujifunzaji wa L2. Msingi wake ni kuwa, L1 huathiri ujifunzaji wa L2 na

husababisha vipengele vya kiisimu vya (L1) kuingia L2. Nadharia (tete) hii ina mitindo miwili, ule ulio mkali na ulio wa wastani. Mtindo mkali unashikilia kuwa, vipengele vyote vinavyoweza kumtatiza mjifunzaji wa L2 kutoka L1 vinaweza kutabiriwa kwa kulinganisha L1 na L2 ili kubainisha vipengele vinavyofanana na vile vinavyotofautiana kati ya lugha hizi. Kwa mtindo huu, vipenegele vilivyomo katika L1 vinavyofanana na vya L2 vitamwezesha mtu kujifunza L2 kwa urahisi na vile ambavyo havimo katika L1 na vimo katika L2 vitamtatiza katika mchakato wake wa kujifunza L2 (Choge, 2016, p. 35). Naye Wardhaugh (akirejelewa katika Jajareh 2015, p. 1111) anaeleza kuwa, mtindo wa wastani unashikilia kuwa, athari za L1 katika ujifunzaji wa L2 haziwezi kutabirika kwa kubainisha sifa zinazofanana na kutofautiana kati ya L1 na L2 kupitia ulinganisho, bali, kwa kuchunguza matokeo ya lugha ya mjifunzaji wa L2. Utafiti wa makala hii ulichukua mtindo huu wa pili ambao uliwezesha utafiti huu kutambua sifa za kimfosintaksia zilizowaathiri wanafunzi wanaosema Kinandi kama L1 katika ujifunzaji wao wa Kiswahili kama L2 kwa kuchunguza tungo zao kengeushi walizozalisha katika insha zao. Utafiti huu ulilinganisha tungo sanifu za Kiswahili, Kinandi na zile kengeushi ili kubainisha vipengele vya mfumo wa vihusishi vilivyosababisha ukengushi wa tungo katika insha za wanafunzi wa NSB. Sehemu ifuatayo ya makala hii imeripoti athari za mfumo wa vihusishi wa Kinandi katika insha za wanafunzi hao.

### **Athari za mfumo wa vihusishi wa Kinandi katika insha za wanafunzi wanaosema Kinandi kama L1**

Matumizi ya vihusishi katika insha ni mojawapo ya mifanyiko ya kimfosintaksia iliyowapa changamoto nyingi takriban wanafunzi wote wa shule za msingi za NSB katika uandishi wao wa insha za Kiswahili. Waliathiriwa na mfumo wa vihusishi wa Kinandi. Athari hizi zilidhihirika kwa namna tatu zifuatazo, wanafunzi kukosa kuvitumia vihusishi katika miktadha iliyohitajika, kuvitumia katika miktadha visipohitajika na kuvitumia visivyofaa katika miktadha iliyotumiwa. Uchanganuzi wa kila jinsi unafuata.

**Kutotumia vihusishi katika miktadha ilipohitajika kutumiwa**

Idadi kubwa ya wanafunzi hao wa shule za msingi katika Kaunti ya Nandi nchini Kenya walikosa kutumia kihusishii *katika* na kisawe chake {-ni} katika miktadha ambayo vihusishi hivi vilihitajika. Walikosa kutumia *katika* mwanzoni na katikati mwa tungo japo kihusishi hiki kinahitajika katika miktadha hii katika Kiswahili. Ifuatayo ni mifano ya tungo kengeushi kutoka insha za wanafunzi wa NSB zilizo na ukosefu wa vivumishi hivi: *chumba cha kulala kuna kitanda, taa.....na Shule ya xyz kuna walimu*. Kutotumia kihusishi hiki kunatokana na athari za mfumo wa kimofosintaksia wa Kinandi isiyohitaji kihusishi cha mahali katika miktadha hiyo ama huenda matumizi yake ni ya hiari jinsi ilivyo kwa matumizi ya kihusishi cha mahali mwanzoni mwa sentensi. Jedwali lifuatayo linaonyesha uchanganuzi kimofosintaksia wa tungo kengeushi *chumba cha kulala...* uliofanywa kiulinganishi kati yake na visawe vyake sanifu katika Kiswahili na Kinandi (Choge, 2016, p. 146).

Jedwali 2: *chumba cha kulala...*

Msimbo	KH	F-N			F-U/	F-T
		umoja	mzizi	umoja	F-H	
Kiswahili sanifu	<b>katika</b>	ch-	umba	∅	cha	kulala...
Tungo Kengeushi	∅	ch-	umba	∅	cha	kulala...
Kinandi sanifu	i. ∅	∅	rum-	-it	ne	kirwei...
	ii. <b>eng</b>	∅	rum-	-it	ne	kirwei...
Tungo sanifu:		<i>katika chumba cha kulala...</i>				

kutoka Choge (2016, p. 147)

Uchanganuzi kimofosintaksia wa tungo kengeushi katika jedwali 2 imedhihirisha kuwa, nafasi ya kihusishi *katika* ni kapa {∅} kama ilivyo katika tungo (i) ya Kinandi. Hali hii ni tofauti na ilivyo katika tungo ya Kiswahili sanifu ambayo nafasi ile ya {∅} imekaliwa na kihusishi *katika* mwanzoni mwa tungo kama ilivyo kihusishi *eng* katika tungo (ii) ya Kinandi. Hii inadhihirisha kuwa, kukosa kwa

wanafunzi hao kutumia kihusishi *katika* mwanzoni mwa tungo zao kulitokana na athari za mfumo wa kimfosintaksia wa Kinandi usiohitaji vihusishi kutumiwa mwanzoni mwa tungo. Japo ni suala la faradhi kutumiwa kwa kihusishi katika muktadha huu katika Kiswahili, matumizi yake ni suala la suna katika Kinandi.

Vile vile, Choge anaeleza kuwa kutokana na athari za Kinandi, baadhi ya wanafunzi wa NSB walikosa kutumia kihusishi hiki ndani ya tungo zilizohitaji matumizi yake. Ifuatayo ni mifano ya tungo za aina hii: ...*niko shule ya msingi ya...(...xyz...)*, ...*tukiwa kiwanja tunajesa mjeso ya kandanda na lakini walitushinda mchezo wafalibali*. Jedwali lifuatayo linaonyesha kiulinganishi muundo wa tungo kengeushi ...*niko shule* (Choge, 2016, p. 147).

Jedwali 3: ... *niko shule ya...*

Msimbo	F-T		F-H	F-E	
	kiwakilishi	Kitenzi kishirikishi	kihusishi	nomino kihusishi	
Kiswahili sanifu	i.	ni-	-ko	<b>katika</b> shule -	
	ii.	ni-	-ko	- shule- <b>-in</b>	
Tungo kengeushi	ni-	-ko	∅	shule ∅	
Kinandi sanifu	a-	-mii	∅	sukuul ∅	
Tungo sanifu:		niko <i>katika</i> shule... ama niko shuleni...			

kutoka Choge (2016, p. 148)

Kando na kutotumia kihusishi *katika* ndani ya tungo, wanafunzi hao wa NSB walikosa kutumia alomofu yake {-ni} ambacho ni kihusishi tegemezi nomino. Kihusishi hiki huibadilisha pia nomino kuwa kielezi cha mahali. Kihusishi hiki huzaliwa na mfumo wa sintaksia wa Kiswahili. Mifano ya tungo kengeushi katika insha za wanafunzi hao zilizohitaji mofu hii lakini wanafunzi hao walikosa kuiambisha ni: ...*wananiipenda kwa sababu nachikaza masomo∅, msichana alitia nta masikio∅yake...* na *kule korti∅ kijana Yule...* katika Kiswahili sanifu, vielezi hivi vinafaa kuwa *masomoni, masikioni na kortini*. Ukosefu wa kupachika mofu hii

unatokana na athari za Kinandi isiyokuwa na vihusishi tegemezi vinavyoambishwa kwenye nomino kama inavyoonyeshwa katika jedwali 3.

Japo vihusishi vimo katika kundi la mofu mfumo, si lazima vichangiwe na LM pekee, vinaweza kutoka pia LL. Katika miktadha ya tungo hizi, Kinandi ilisababisha kutotumika kwa kihusishi *katika* na alomofu yake {-ni}. Katika Kinandi, dhana ya mahali inayowasilishwa na {-ni} katika Kiswahili, imejengwa ndani ya nomino pasipo kupachikwa mofu zozote. Hii inadhihirisha kuwa, wanafunzi hao katika **Kiwango Dhahania (KD)** walikuwa wakitumia mfumo wa Kinandi walipotumia nomino hizi bila kihusishi {-ni} kinachotumiwa katika Kiswahili kugeza nomino kuwa kielezi cha mahali. Fikirani mwa wanafunzi hao, tungo hizi zilikuwa sahihi kwa kuwa walikuwa wameathiriwa na mfumo wa Kinandi usiohitaji vihusishi hivi. Haikuwajia katika utambuzi wao kuwa, hawajawasilisha dhana ya undani jinsi inavyohitajika katika Kiswahili Sanifu, Wao walidhani kuwa, wamewakilisha dhana ya undani wa kitu kama ilivyo katika Kinandi pasipo kutumia *katika* ama {-ni}.

Aidha, wanafunzi hao walitumia vihusishi hivi viwili *katika* na {-ni} katika miktadha ambayo kimoja pekee kilihitajika. Mifano ya tungo kengeushi yenye matumizi haya ni: *watoto **katika nyumbani** wanaenda shuleni* ya ...xyz... na *Tuliingia **katika hotelini** mkubwa*. Matumizi ya vihusishi hivi yanadhihirisha kuwa, kisaikolojia wanafunzi hao wamechukulia kuwa nomino zilizo na kihusishi (-ni) ni mofu huru na kwao, kihusishi pekee ni *katika*. Kutotumika kwa mofu hii ni kutokana na athari ya mfumo wa kimofosintaksia ya Kinandi usio na mofu tegemezi mahali kinachoambishwa kwa nomino, kwa hivyo akili zao hazitambui kihusishi {ni} katika F-N hizi (Tazama jedwali 3).

Wanafunzi hao vilevile, walitatizika katika kutumia vihusishi *kwa, kutoka* na *kwenye*. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya tungo ambazo wanafunzi hao walitumia vihusishi hivi kikengeushi: *baada ya kumaliza ibaada **kwa** kanisa, alikuwa mshindi **kwa** mtihani wake, pete hiyo ilikuwa imeundwa **kutokana** na dhahabu* na



...tume panda miti mingi sana **kwa** shule yetu. Jedwali lifuatayo linaonyesha tungo hizi kengeushi na hali zao sanifu katika Kiswahili na Kinandi.

Jedwali 4 Tungo kengeushi kutokana na matumizi ya vihusishi visivyofaa muktadha

Msimbo	na	Tungo kengushi na visawe vyazo	Vihusishi husika
Kiswahili sanifu		Baada ya kukamilisha ibada Ø kanisani...	{-ni}
Tungo kengeushi	1	Baada ya kumaliza ibada <b>kwa</b> kanisa...	kwa
Kinandi sanifu		Ye kaangoporok saet <b>eng</b> kanisa...	eng
Kiswahili sanifu		...alikuwa mshindi <b>katika</b> mtihani wake.	katika
Tungo kengeushi	2	...alikuwa mshindi <b>kwa</b> mtihani wake.	kwa
Kinandi sanifu		...ki kapeliin <b>eng</b> testi ne nyii.	eng
Kiswahili sanifu		Pete hiyo ilikuwa imeundwa <b>kwa</b> dhahabu	kwa
Tungo kengeushi	3	Pete hiyo ilikuwa imeundwa <b>kutokana na dhahabu.</b>	kutokana na
Kinandi sanifu		Peteiyondonoto kokikakiae taabu.	-e

kutoka Choge (2016, p. 151)

Kinandi kina kihusishi *eng* ambacho kinatumika kutekeleza dhima tofauti ambazo Kiswahili ingetumia aina tofauti za vihusishi. Kihusishi hiki kina kisawe {-e} ambacho ni mofu tegemezi inayoambishwa tamatini mwa fungutenzi na vitenzi kama ilivyo katika kitenzi *kokikakiae* ambayo tafsiri yake ni *'ilikuwa imetengenezewa...'* kitenzi *ai* *'tengeneza'* kikipachikwa kihusishi tegemezi {-e} inaunda fungutenzi *ae* lenye maana ya *tengenezewa*. Vihusishi hivi vinatumiwa kwa miktadha yote, *eng* ikitumiwa kuwasilisha dhana za wakati na mahali, nayo {-e}, kuwasilisha dhana za miondoko, kisababishi na kitumizi.

Kando na hayo, baadhi ya wanafunzi wa NSB walitumia vihusishi *kwa*, *kutoka* na *kwenye* katika miktadha isivyohitajika na baadhi yao walikosa kuvitumia katika miktadha ambayo vihusishi hivi vilihitajika. Jedwali lifuatalo linatupatia ulinganisho wa tungo kengeushi na visawe vyake sanifu katika Kiswahili na Kinandi. Ukengeushi huu ulitokana na wanafunzi hao wa NSB kutumia kihusishi *kwa* katika muktadha usiofaa.

Jedwali 5: *kwa* shule yetu tuna chikoni...

<i>Msimbo</i>	<i>na</i>	<i>Tungo kengeushi na visawe vyazo</i>	<i>Vihusishi</i>
Kiswahili sanifu	i.	<b>Katika</b> shule yetu mna jikoni...	<b>Katika</b>
	ii.	Shule <b>ni</b> mwetu mna jikoni	<b>-in</b>
<i>Tungo kengeushi</i>		<i>kwa</i> shule yetu tuna chikoni...	<i>kwa</i>
Kinandi sanifu		<b>Eng</b> sukuulit nyoo ko mi chikoni...	<b>eng</b>

kutoka Choge (2016, p. 214)

### **Kuvitumia vihusishi katika miktadha visipohitajika**

Kando na kuzalisha tungo kengeushi kwa kutumia vihusishi visivyofaa katika miktadha, wanafunzi hao walitumia pia vihusishi katika miktadha isivyohitajika kama inavyobainishwa na tungo zifuatazo: *tuliingia katika hotelini mkubwa* na *watoto katika nyumbani wanaenda shuleni* ya.... Wanafunzi hao walitumia kwa pamoja kihusishi *katika* na alomofu yake {-ni} katika tungo moja (Choge, 2016, p. 149). Tungo sahihi zingekuwa: *tuliingia katika hoteli kubwa* na *nyumbani, watoto wanaenda shuleØ* ya... Kulingana na mtindo wa KD, akili za hao wanafunzi hazikutambua matumizi ya vihusishi hivi kwa kuwa, walizalisha tungo hizi kwa kutumia mfumo wa kimofosintaksia wa Kinandi usio na kihusishi tegemezi cha mahali kinachoambishwa kwa nomino na vilevile, si lazima katika Kinandi kutumia vihusishi mwanzoni mwa tungo.

**Kutotumia vihusishi katika miktadha iliyohitajika kutumiwa**

Kando na kutumia vihusishi katika miktadha ambayo havikuhitajika, wanafunzi hao pia walikosa kuvitumia vihusishi hivi katika miktadha ambavyo vilihitajika. Mifano ya tungo hizo kengeushi kutokana na kutumia vihusishi ni: ...*alienda nyumbani akakaa mwezi moja...* na ...*lilikuwa likipita kazi*. Jedwali lifuatayo linaonyesha ulinganisho kati ya tungo hizi kengeushi na visawe vyazo sanifu katika Kiswahili na Kinandi.

*Jedwali 6: ...ilikuwa likipita kazi na ... akakaa  $\emptyset$  mwezi moja...*

<i>Msimbo</i>	<i>na.</i>	<i>Tungo kengeushi na visawe vyazo</i>	<i>vihusishi</i>
Kiswahili sanifu		...lilikuwa likipita <b>kwa</b> kasi.	kwa
<i>Tungo kengeushi</i>	<b>1</b>	... <i>lilikuwa likipita <math>\emptyset</math> kazi.</i>	$\emptyset$
	i	...ne kisirtoi <b>eng</b> sipiit	eng
Kinandi sanifu	ii	...ne kisirtoi $\emptyset$ sipiit	$\emptyset$
Kiswahili sanifu		...alienda nyumbani akakaa <b>kwa</b> mwezi moja...	kwa
<i>Tungo kengeushi</i>	<b>2</b>	... <i>alienda nyumbani akakaa <math>\emptyset</math> mwezi moja...</i>	$\emptyset$
Kinandi sanifu		...kiwo hгаа ipkotebi $\emptyset$ araweeet akenge	$\emptyset$

kutoka Choge (2016, p. 151)

Katika jedwali 6, tungo kengeushi **na.1** ina visawe viwili katika Kinandi. Kisawe kimoja 1(i) kimetumia kihusishi *eng* na cha pili 1(ii) hakikutumia kihusishi chochote, ni  $\{\emptyset\}$ . Tungo kengeushi **na.2** haikutumia kihusishi chochote, pia ni  $\{\emptyset\}$ . Mifano hii inaonyesha kuwa, katika mfumo wa kimofosintaksia ya Kinandi, si lazima vihusishi vitumiwe ili tungo iwe sanifu. Mifano hii imedhihirisha pia kuwa, ukengeushi wa tungo za wanafunzi wa NSB katika jedwali 6 ulitokana na kuathiriwa na mfumo wa kimofosintaksia ya Kinandi kuhusiana na matumizi ya vihusishi.

**Hitimisho**

Makala hii imeonyesha kuwa, mfumo wa kimofosintaksia wa vihusishi vya Kinandi uliwaathiri wanafunzi wa shule za NSB wanaosema Kinandi kama L1 katika

matumizi ya vihusishi vya Kiswahili sanifu katika insha zao. Matokeo ya uchunguzi huu yameipatia mashiko nadharia ya mtindo wa mfumo-jozi ulioasisiwa na Kecskes (2006, p. 257) inayoelezea kuwa, lugha zote za mjozi-lugha huunda mfumo mmoja unaongoza matumizi ya kila moja ya lugha zake. Uteuzi wa lugha ya kuzalishia mawasiliano hufanyika akilini mwake kwa kutumia kifaa mfano wa swichi. Wakati mjozi-lugha anapotumia mojawapo ya lugha zake, zile lugha zingine huchochewa pia. Uchochezi huo husababisha lugha hizi kutagusana na kuathiriana kiisimu, mwingiliano huu ukisababisha baadhi ya vipengele vya kiisimu vya lugha hizi kuingiliana bila utambuzi mjozi-lugha japo kwa ufahamu wake ameiteua lugha moja ambayo anaitumia kwa mawasiliano. Katika mtindo wa MLF na KD mnenaji/mzalishaji tungo kila mara yumo katika harakati za kuteua mifumo ya lugha anayotumia kuzalishia tungo zake. Yeye huteua akilini mwake mfumo lugha utakaoongoza muundo wa ndani wa tungo zake aghalabu bila utambuzi wake na huteua kimaksudi lugha itakayoipa tungo hizi umbo la nje. Makala hii imedhihirisha kuwa, wanafunzi wa NSB waliathiriwa na mfumo wa kimofosintaksia wa vihusishi vya Kinandi. Hivyo basi, ni muhimu kwa mwalimu wa L2 awe na tajiriba katika isimu ili aweza kuzikabili vyema athari za kiisimu za L1 kabla hazijalemaza uamiliaji wa L2 jinsi athari za Kinandi zilivyofanya kwa uamiliaji wa Kiswahili kama L2 miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi wa NSB. Matawi ya isimu yaliyo muhimu kwa mwalimu anayefunza L2 ni: Isimu peke, isimu-nafsia, isimu-migusano, isimu-linganishi na uamiliaji wa L2. Vilevile, waalimu wanaofunza wanafunzi ambao L1 zao ni za jamii tofauti za lugha jinsi Kinandi na Kiswahili zilivyo-Kinandi ikiwa ni ya jamii ya kinile na Kiswahili kibantu-wanafaa kujua mifumo ya kimofosintaksia ya lugha hizi ili waweze kusaidia wanafunzi wao kutambua na kuzikabili vyema changamoto za kimofosintaksia kutoka L1 zinazowakabili katika uamiliaji wao wa L2.

### **Maelezo ya istilahi na vifupisho**

- F-N:** Fungu changamano la **Nomino**
- F-T:** Fungu changamano la **KiTenzi**
- F-H:** Fungu changamano la **KiHusishi**
- F-U:** Fungu changamano la **kiUnganishi**

**F-E:** Fungu changamano la kiElezi  
**n.w** na wengine

### Marejeleo

- Al-khresheh, M. H. (2016). A Review Study of Contrastive Analysis Theory. *Journal of Advances in Humanities and Social Sciences*, 2 (6), 330-338
- Choge, S. (2018). Nafasi ya Nadharia ya Myers-Scotton katika Uchanganuzi wa Matokeo ya Mitagusano ya Lugha katika Kiwango cha Kimofosintaksia. *Lugha ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo yake* (pp. 109-119). Dar esalaam: TUKI.
- Choge, S. C.(2016). *Morphosyntactic Analysis of Kinandi L1 Speaking Pupils' Kiswahili Essays as an Insight into Psycholinguistic Challenges of 2<sup>nd</sup> Language Acquisition*. 2016. (Tasnifu ya Uzamili, haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Moi, Eldoret, Kenya
- Dost, I. N. & Ghassem, B. (2017). *A Review Of Contrastive Analysis Hypothesis With A Phonological And Syntactical View: A Cross-Linguistic Study*. *The Buckingham Journal of Language and Linguistics*. 1, 32-41.
- Kecskes, I. (2006). *The dual language model to explain codeswitching: A cognitive-pragmatic approach*. *Intercultural Pragmatics*, 3 (3).257–283. DOI 10.1515/IP.2006.017
- Krashen, S. D. (2009). *Principles and Practice in Second Language Acquisition* (Internet Edn.), Retrieved September 25, 2019 (<http://sdkrashen.com/Principles and Practice/Principles and Practice.pdf>) (Original work published 1982).
- Mwangi, S. (2003). *Prepositions in Kenyan English. A Corpus-Based Study in Lexico-Grammatical Variation*. Aachen: Shaker Verlag.
- Myers-Scotton, C. (2001a). Explaining Aspects of Code-Switching and Their Implications. In J.K. Nicol (Ed.), *One Mind Two Languages. Bilingual Languages Processing* (pp 84-115). Maiden, MA: Blackwell
- Myers-Scotton, C. (2002). *Contact Linguistics. Bilingual Encounters and Grammatical Outcomes*. Oxford: Oxford University Press

- Myers-Scotton, C. (2008). Language Contact: Why Outsider System Morphemes Resist Transfer. *Journal of language contact*, 2.(1), 21-41. Doi 10.1163/000000008792525318
- Tajareh, M. J. (2015). An Overview of Contrastive Analysis Hypothesis. *Cumhuriyet Üniversitesi Fen Fakültesi Fen Bilimleri Dergisi (CFD)*. 36 (3). ISSN: 1300-1949
- van Els, Bongaerts, T., Extra, G., van Os, C., & van Diäten, AM. J. (1984). *Applied Linguistics and the Learning and Teaching of Foreign Languages* (R.R.van Oirsouw). London: Edward Arnold. (original work published 1977).
- Yule, G. (2010). *The Study of Language*. (4<sup>th</sup> Edn). Cambridge: Cambridge University Press. [www.cambridge.org/9780521765275](http://www.cambridge.org/9780521765275).
- Mwandishi anukuu vyanzo kutokana na majarida inavyostahili – italiki itumiwe kuonyesha jina la jarida na wala siyo anwani ya makala.